WIZARA YA ELIMU,SAYANSI,TEKINOLOJIA NA UFUNDI.
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGOMA UJIJI.

SHULE YA SEKONDARI MLOLE
S.L.P 96,
KIGOMA.
Tarehe …….

Simu: 0766642156.
Kumb.Na.ML. SS/F.01/19.

JINA LA MWANAFUNZI…….
S.L.P…….
KIGOMA.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MLOLE MWAKA 2020.

1.0 Utangulizi.

Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2020 katika shule hii. Shule ya sekondari Mlole ni ya kutwa, iko km 5 kutoka mjini kata ya Gungu mtaa wa Gezaulole karibu na chuo cha VETA.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021, kwa hiyo unatakiwa kuripoti shuleni mapema tarehe 11/01/2021 saa 1:30 asubuhi bila kuchelewa.

Mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021, baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa shuleni.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1 Sare za shule.

a. Wavulana.

i. Shati nyeupe mbili (tetroni) mikono mifupi zisizobana mikono wala kiuno.

ii. Suruali rangi ya kahawia mbili, ziwe na linda mbili,mifuko mitatu zisizobana (modo) ukija na suruali ya kubana hutapokelewa shuleni

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba) visiwe raba.

iv. Soksi nyeupe fupi pea mbili

v. Mkanda wa rangi ya kahawia au nyeusi, wenye chuma kidogo kisichokuwa na malembo yoyote.

b. Wasichana.

i. Shati nyeupe mbili (tetroni) mikono mifupi zisizobana mikono wa kiuno.

ii. Sketi mbili rangi ya kijivu zenye malinda 14 urefu unaopita magoti sentimeta 15.

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba) visiwe raba

iv. Soksi nyeupe (stoking) angalau pea mbili.

v. Wanaopenda kuvaa hijabu wanatakiwa kushona hijabu ndefu inayovuka kiwiko cha mkono rangi nyeupe, na isiwe na malembo yoyote.

c. Nguo za micheza.

i. Wavulana.

a. Bukta nyeupe

b. Raba

c. Fulana rangi ya zambarau isiyo na maandishi**.**

ii. Wasichana

a. Sketi nyeusi

b. Raba

c. Fulana rangi ya zambarau isiyo na maandishi**.**

d. Vifaa vya Taaluma.

i. Daftari kubwa (counter books) kumi

ii. Mkebe wa mahesabu (mathematical set)

iii. Dictionary ya Kiingereza kwa Kiswahili (English-Swahili)

SHERIA ZA SHULE.

Kila mwanafunzi analazimika kuzifuata sheria na kanuni za shule hivyo ni marufuku:

1. Kuiba au kusaidia wizi utendeke
2. Kuwa muasherati, kubaka au kujaribu kubaka au kuwa shoga
3. Kutumia vilevi kam vile pombe, bangi, cocaine, heroin, n.k
4. Kuvuta sigara au ugoro
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6. Kufuga nywele ndefu, kucha na ndevu
7. Kuvaa bangili, kupaka madawa kwenye nywele, kupaka rangi kwenye mdomo.
8. Kutofanya mitihani au majaribio
9. Kukataa adhabu ya mwalimu/mlezi/kiranja kwa makusudi
10. Kupiga au kupigana
11. Kudharau bendera ya taifa
12. Kuoa au kuolewa
13. Kugoma au kuchochea mgomo ufanyike
14. Kupata mimba au kusababisha mimba
15. Kutoa mimba
16. Kutoroka vipindi au kukwepa kazi za nje ya darasa kwa makusudi.
17. Kujibizana au kufokeana na mwalimu/mlezi na kuonyesha kiburi
18. Kutoa lugha ya matusi kwa mwanafunzi mwenzako,mwalimu au kiranja
19. Kuvaa sare bila nidhamu kwa mfano
    a. Kutochomekea shati au fulana
    b. Kudebedesha suruali
    c. Kukunja suruali au sketi kwa kisingizio cha kuwa ndefu.
20. Kutinda nyusi, kuvaa hereni, kunyoa panki au kipara.
21. Kwenda nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu.
22. Kuchelewa shuleni bila sababu ya msingi
23. Kujihusisha na harakati za kidini zenye mwenendo wa kuleta ubaguzi na chuki shuleni.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.

i. Wizi
ii. Uasherati, ubakaji na ushoga
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
iv. Makosa ya jinai
v. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi
vi. Kudharau bendera ya taifa
vii. Kuoa au kuolewa
viii. Kupata mimba, kutoa mimba, au kusababisha mimba
ix. Kugoma au kuchochea mgomo au kushiriki kuvuruga amani na utulivu wa shule
x. Kukataa adhabu ya mwalimu, mlezi au kiranja.
xi. Utoro wa bila taarifa
xii. Kuwa na simu ya mkononi shuleni

NGUZO NA MWENENDO WA SHULE.

1. HESHIMA NA UTII.
   a. Kila mwanafunzi awaheshimu wenzake, walimu, walezi au watu wengine anaokutana nao ndani na nje maeneo ya shule.
   b. Kila mwanafunzi awahi kila mahali anapohitajika hasa anapoitwa na mlezi au kengele.
2. USAFI NA AFYA.

   Mwanafunzi haruhusiwi kufuga nywele ndefu, ndevu wala kusuka nywele mtindo wa aina yoyote

3. MAVAZI
   a. Kila mwanafunzi avae mavazi ya heshima yaliyo safi
   b. Shati lichomekewe ndani ya suruali na ndani ya sketi muda wote ndani na nje ya mipaka ya shule

4. RUHUSA.

   Hairuhusiwi mwanafunzi kwenda nje ya mipaka ya shule bila ya ruhusa ya mwalimu.

NYOGEZA

Fomu zifuatazo zimeambatishwa ili zijazwe na kuletwa shuleni mwanafunzi anaporipoti shuleni.

1. Historia ya mwanafunzi na familia yake (FOMU A)
2. Fomu ya uchunguzi wa kitabibu (FOMU B). Fomu hii hujazwa hospitali ya serikali
3. Affidavit Form (Form C) Fomu hii hujazwa mahakamani na wanafunzi ambao hawana vyeti vya kuzaliwa tu. Wanafunzi wenye vyeti vya kuzaliwa hawajaza fomu hii bali wataleta nakala (copy) za vyeti vyao vya kuzaliwa.

KANDIDUS R.KAMAZE
Kaimu Mkuu wa Shule.

HEADMASTER
MLOLE SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 96
KIGOMA

FORM A.

HISTORIA YA MWANAFUNZI NA UKOO WAKE.

1. Jina la mwanafunzi……
2. Dini……Tarehe ya kuzaliwa……
3. Jina la baba mzazi/mlezi unayeishi naye……
   Kazi yake……
   Simu……
4. Jina la mama mzazi/mlezi unayeishi naye……
   Kazi yake……
   Simu……
5. Habari za jamaa na familia wanaoweza kusaidia wakati wa matatizo.

Na	JINA KAMLI	UMRI	UHUSIANO	KAZI YAKE	SIMU
1					
2					
3					

Wahusika waliotajwa hapo juu ndio pekee watakaotambulika rasmi na uongozi wa shule pindi panapotokea jambo lolote la msingi linalohitaji mzazi/mlezi.

RIDHAA YA MZAZI/MLEZI KURIDHIA MWANAE KUJIUNGA NA SHULE HII.

Mimi……ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi……nakiri kuwa nimesoma na kuzielewa sheria zote za shule na ninaahidi kuwa nitamuhimiza mwanangu azifuate sheria zote kwa ukamilifu.

Sahihi…… Tarehe……

KIAPO CHA MWANAFUNZI KUKUBALI/KUTOKUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE.
Mimi……nakiri kuwa nimezisoma na kuzielewa sheria zote za shule na hivyo **ninakubali/sikubali** kujiunga na shule hii na ninaahidi kuwa nitazifuata sheria zote za shule kwa ukamilifu.
Sahihi……Tarehe……

FORM B

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

MLOLE SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 96 KIGOMA

To be completed by a medical officer in respect of all form one entrants.

Pupil's name in full……

Age……Sex……

Blood found (Red and White)……

Stool examinations……

Urine analysis……

Syphilis and other venereal diseases test……

……

T.B Test……

Eye Test……

Ears Test……

Chest……

Spleen……

Abdomen……

Pregnancy test (girls only)……

Any other (physical defects,impairments,chronic diseases) please specify……

……

……

I certify that I have personaly examined the above named and so do affirm that he/she fits to pursue secondary education as stated above.

Signature……

Designation……

Station……Stamp……

Date……

Kumbuka: Huduma hii inalipiwa hivyo hakikisha umelipia na umepewa risiti ya malipo na uiambatanishe na fomu hii pindi unapokuja shuleni.

FORM C

AFFIDAVIT FORM

(Section 10)

Date and place of birth……

1.1 ……

(Full name of the person taking asking declaration)

2. Age……solemnly and sincerely declares that I am the father/mother or near relative of ……

(state full name)

3.That the said……

Was born on……Day of……Year……

That I remember the occasion as I was present shortly after his/her birth.

I the said……

Make this declaration concern by believing the name to be true and in accordance with the provisions of the oaths (Judicial Proceedings) and Statutory Declaration act o 1996.

……

(Signature of the person making declaration.)

MAGISTRATE/COMMISSIONER FOR OATHS.

This declaration is made and subscribed by the said

……who is known to me personally or identified to me by ……or latter being known to me personally this ……day of……year……

Signature……

Qualification……

Address……

……

……

Official rubber stamp.